Pierre de Coubertin

Mwana Historia Mwenye Mtazamo Wa Mbali

Coubertin mwenyewe aliunda kimsingi masomo mengi ya kihistoria na kutumia ustadi wake wa historia kukadiria ipasavyo matukio ya hapo maajuzi. Kwa mujibu wa Coubertin, upanuzi wa mawazo ya kihistoria ni muhimu sana. Ana wazo kwamba thamani ya tamaduni zilizopuziliwa na historia zingefundishwa mapema ili kuongeza maendeleo ya kijamii/kukua kwa jamii. Kusema kweli kutojua na kutokujua kulisababisha balaa nyingi na vita. Coubertin aliitazama historia kama mlinzi wa amani ya kimataifa.

"Nimewahubiria kuhusu spoti na historia yapata sasa robo ya karne; mmesikia wito wa mazoezi ya viungo, chanzo cha nguvu za kiviungo na kimaadili kwa pamoja (...). Lakini hamjasikia wito wa utamaduni wa kihistoria. Msidhani nimekata tamaa nitaendelea kulitangaza na kulihubiri hadi pumzi yangu ya mwisho (kifo)."



1926-27 Coubertin alichapisha " Historia ya Ulimwengu" yenye juzuu nne.

Mada zifuatazo huonyesha uchangamano na mtazamo mbali na masomo yake:

"Waelekea wapi Uropa?", tayari 1923 (!); "Historia ya karne ya XX"; "Historia ya Amerika Kusini"; "Charlemagne na ufalme wake"; "Mateka wa meli - The Vikings"; "Historia ya Amerika"; "Tujifikirieje kuhusu ujamaa?"; "Mageuzi ya kijamii"; "Elimu ya amani"; "Maswali ya kifedha"; " Kufufuka kwa watu"; "Mtazamo wa Wafaransa kwa ufalme wa kijerumani"; "Uhispania na binti zake"; "Pumziko la Australia"; "Poland Iisilojulikana"; "The Conditions of Scandinavian Progress"; "Ethiopia leo"; "Na mwisho wa Urusi", "Sanaa ya Kiarabu na mengine mengi.

Copyright Pierre-de-Coubertin-Gymnasium Erfurt